

Maswali

1. Mungu aliahidi Abramam nini?
2. Mbona Abramam na Sarai walikuwa na wasiwasi?
3. Sarai alifanya nini?
4. Mungu alimwambia Hajiri nini alipotoroka?
5. Mungu alimwambia Abramam nini juu ya Ishmaeli?
6. Mungu alimpa Sarai nini?
7. Mbona Sarai alitaka Ibrahimu afukuze Ishmaeli?
8. Ibrahimu alifanya nini?
9. Mungu aliwaokoa Hajiri na Ishmaeli namna gani?
10. Familia ya Ishmaeli ya sasa inaitwaje?

Majibu

1. Mungu alimwahidi Abramam kwamba atakuwa na familia kubwa.
2. Abramam na Sarai walikuwa na wasiwasi kwa sababu Sarai hangeweza kupata watoto.
3. Sarai alimpa Abramam mjakazi wake ili amzalie watoto.
4. Mungu alimwambia Hajiri arudi kwa sababu mwanawe atakuwa taifa kubwa.
5. Mungu alimwambia Abramam kwamba hajachagua Ishmaeli lakini bado Ishmaeli atakuwa taifa kubwa.
6. Mungu alimpa Sara mwana aitwae Isaka.
7. Sara alitaka Ibrahimu afukuze Ishmaeli kwa sababu alimchokoza Isaka.
8. Ibrahimu aliomba Mungu halafu akafukuza Hajiri na Ishmaeli.
9. Mungu aliwaokoa Hajiri na Ishmaeli wasikufe kwa kufanya kisima jangwani.
10. Familia ya Ishmaeli ya sasa inaitwa Waarabu.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 1 Mwaka wa 2



2 Hajiri na Ishmaeli

Marejeo

Mwanzo 16, 17: 18 – 22, 21

Kiini cha somo

Kuonyesha vile Abramam alijaribu kutatua shida bila Mungu. Alifanya shida ikawa mbaya zaidi.

Maneno maalum

1. Mungu anahidi Abramam familia + hakuna mtoto.
2. Sarai + Hajiri + mtoto mchanga
3. Rudi + Ishmaeli + taifa kubwa + mtu mmitu
4. Mwana wa Sarai + sio Ishmaeli + majina yanabadilika.
5. Isaka + Ishmaeli mmbaya
6. Mungu atalinda Ishmaeli + fukuza
7. Hakuna maji + Mungu aahidi+okoka.
8. Kua + oa Mmisri + watoto 12 + Waarabu.

2.1 BWANA alifanya agano. Aliambia Abramam angalia nyota angani. Abramam hangeweza kuzihesabu. Mungu akasema, “Hata kwa siku zijazo, hakuna atakayeweza kuhesabu familia yako!” Lakini Sarai hakuweza kupata watoto. Abramam na Sarai walishangaa vile ahadi ya Mungu itatimizwa.

2.2 Sarai akampa Abramam Hajiri mjakazi wake ili amzalie watoto. Hawa watoto wangeanzisha familia kubwa aliyoihidi Mungu. Mda mfupi Hajiri akijua atapata mtoto, akajiona ni wa maana kuliko Sarai. Sarai hakumpenda na akawa mbaya kwa Hajiri. Kwa hivyo Hajiri hakufurahia na akatoroka.

2.3 Mungu akatuma malaika amwambie Hajiri arudi. Ataita mwanawe Ishmaeli. Mungu atafanya familia yake kubwa lakini atakuwa mtu mwa kubishana na watu wengine. Hajiri alirudi kwa Abramam na akazaa Ishmaeli.

2.4 Mungu alinena na Abramam tena. Akasema, “Sarai atazaa mwanawe na ataitwa Isaka. Isaka ndiye mwana niliye kuahidi, sio Ishmaeli.”

Kama ishara Mungu alibadilisha majina ya Abramam na Sarai. Wakaitwa Ibrahimam na Sara.


2.5 Ishmaeli alipokuwa na miaka 14, Mungu alimpa Sara mwana na akamwita Isaka, vile aliambiwa na Mungu.

Ishmaeli alikuwa mbaya kwa Isaka akimchokoza. Sara hakufurahia na akamwambia Ibrahimam amfukuze.

2.6 Ibrahimam alihuzunika. Alimpenda Ishmaeli. Na akataka Mungu amwambie cha kufanya. Mungu alimwambia, “Fanya vyenye Sara amekwambia. Nimechagua familia ya Isaka kuwa watu wangu. Lakini nitamshugulikia Ishmaeli pia.”

Kwa hivyo Ibrahimam alimwachilia Hajiri na Ishmaeli waende.

2.7 Walipoenda wakatotea na kuishiwa na maji, Hajiri alifikiri kwamba watakufa. Akalala chini na kulia.



Malaika akamwita, “Usiwe na wasiwasi! Nimesikia kilio chako. Nitamlinda mwanao. Familia yako itakuwa kubwa!” Hajiri alinua macho na kuona kisima. Mungu akawaokoa.

2.8 Ishmaeli alikua jangwani. Akawa mpiganaji mkuu. Aliaoa Mmisri. Walipata watoto 12. Familia ya Ishmaeli ndio Waarabu wa leo. Bado wanapigana na familia ya Isaka, ndio Wayahudi.